

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE**

SIMU NA.0768-806119
0756-099456
0757-255004

KUMB. NA.
KWA:

**SHULE YA SEKONDARI ISONGOLE,
S.L.P. 222,
TUKUYU**

**YAH: MAAGIZO NA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA
MWAKA 2021**

Ninayo furaha kubwa kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujunga na kidato cha Kwanza mwaka 2021 katika shule hii. Nakupongea sana kwa kuchaguliwa na nategemea utaitumia nafasi hii ipasavyo ili kujenga historia nzuri ya maisha yako katika nchi hii na popote utakapojaliwa kuishi. Ni mategemeo yetu kuwa utashirikiana vizuri na waalimu, wafanyakazi wasio waalimu, na wanafunzi wenzako kufanyakazi za darasani na nje ya darasa. Unatakiwa kufika shulenii tarehe 11/01/2021 ili kuanza masomo rasmi na kwa wakati. Ukichelewa utaipoteza nafasi hii adimu.

MAHITAJI MUHIMU SHULENI:

Ada na michango yote isipokuwa ya fedha ya maendeleo ilipwe Benki kwa kutumia kumbukumbu zifuatazo:

- 1. MAHITAJI YA KITAALUMA:**
 - ❖ Daftari 5 za kawaida na kaunta 4 (Quire 1). Kalamu, na mkebe 1.
- 2. VIFAA VYA USAFI:**
 - (i) Jembe lenye mpini (ii) Mfagio (chelewa) (iii) Ndoo moja mpya ya ujazo wa lita kumi (10)
- 3. SARE ZA SHULE:**
 - (a) WAVULANA:**
 - ❖ Shati nyeupe mikono mifupi (tetroni) 2, Sweta rangi ya bluu 1 la INDIA AU KENYA na imara, Suruari dark blue 1 na damu ya mzee 1,
 - ❖ Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba visivyo chongoka, Soksi nyeusi jozi mbili (2) au zaidi,
 - ❖ Mkanda mweusi usio na nembo yoyote wala mapambo.
 - (b) WASICHANA:**
 - ❖ Shati nyeupe mikono mifupi (tetroni) 2, Sweta rangi ya bluu 1 la INDIA AU KENYA na imara, Sketi dark bluu 1 na damu ya mzee 1, zote aina ya marinda 12, sita (6) mbele na nane (8) nyuma. Sketi iwe ndefu futi 1 ½ kupita magotii.
 - ❖ Viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba, visivyo chongoka na sio vinginevyo, Soksi nyeupe jozi mbili (2) au zaidi.
- 4. CHAKULA:** kwa mujibu wa muongozo wa elimu bila malipo, ni jukumu la mzazi kuhakikisha mwanafunzi anapata chakula cha mchana ili kupunguza utoro shulenii. Gharama za chakula zitakokana na makubaliano ya kikao cha wazazi/walezi.

KUMBUKA: mzazi utamsimamia mwanafunzi kuhakikisha mahitaji yake yote anapewa na kuhakikisha mahudhurio yake ya kila siku ukishirikiana na walimu.

FOMU MUHIMU UNAZOTAKIWA KUJA NAZO NI HIZI ZIFUATAZO:

- Fomu ya kupimwa afya iliyojazwa baada ya kupimwa na daktari wa hospitali za serikari.
- Cheti cha kuzaliwa.
- Fomu ya tamko la mwanafunzi na mzazi/mlezi iliyojazwa kikamilifu.

KARIBU SANA.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu. Unatakiwa kuzingatia mambo muhimu yafuatayo:

1. Heshima kwa viongozi, walimu, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
2. Mahudhulio mazuri katika kila shughuli za shule na nyngine utakazopewa.
3. Kuwahi kila mahali utakapohitajiwa na kwa wakati.
4. Kujua mipaka ya shule na kuzingatia maelekezo yote juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakti wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
5. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
6. Kuвая sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
7. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
8. Huruhusiwi kuwasha moto wowote ndani ya shule na hata darasani.
9. Mwanafunzi haruhusiwi kabisa kuwa na simu shulenii.
10. Huruhusiwi kuвая mavazi yaletayo aibu kama vile sketi fupi, suruali ya kubana wala nguo yoyote isioyo ya maadili.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

1. Wizi wa aina yoyote.
2. Uasherati, ubakaji, ushoga na kulawiti.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevyaya ya aina yoyote.
4. Uvutaji bangi na sigara.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kujeruhi kwa makusudi.
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
9. Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
10. Kuoa au kuolewa, kusababisha mimba au kupata mimba , au kutoa mimba.
11. Utoro.
12. Kutofanya mazoezi au mitihani ya masomo pamoja na kutega kipindi.
13. Kugoma, kuchochea au kuongoza mgomo.
14. Kukataa adhabu.
15. Kumiliki/kutumia simu shulenii.
16. Kuvuruga amani na utulivu kwa raia ye yoyote wa jamii inayokuzunguka.
17. Kucheza kamali au pool.
18. Kuingia kwenye majumba ya cinema au madangulo.

NB: KUFUATA SHERIA NI LAZIMA WALA SI OMBI.

Tafadhali soma kwa makini maagizo yote na kuyafuata. Karibu Isongole Sekondari

.....
**CHARLES MWANKUGA
MKUU WA SHULE
0768-806119**

**WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI ISONGOLE
S.L.P. 222 TUKUYU**

FOMU YA KUPIMWA AFYA

DAKTARI:

HOSPITALI:

S.L.P.

YAH: KUPIMWA AFYA YA MWANAFUNZI
Tafadhalii tunaomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za mzazi/mlezi wake na uthibitishé kama ataweza kumudu mazingira ya shule hii iliyo eneo la baridi kwa vipimo vifuatavyo:

- ❖ Urine analysis:
- ❖ Stool examination:
- ❖ Syphilis test:
- ❖ Blood count (Red and White):
- ❖ Eye test:
- ❖ T.B. Test:
- ❖ Ear test:
- ❖ Spleen test:
- ❖ Other abnormalities:

Nathibitisha kuwa mwanafunzi mtajwa hapo juu ataweza/hataweza kumudu masomo ya sekondari.

.....
JINA LA DAKTARI

.....
SAHIHI NA MHURI

.....
CHEO

TAFADHARI:

MZAZI/ MLEZI HAKIKISHA MWANAFUNZI ANAPIMWA ILI TUJUE AFYA YAKE NA UDHAIFU WAKE ILI TUWEZE KUMPA HUDUMA NA UANGALIZI WA KARIBU KATIKA KIPINDI CHAKE CHA MASOMO.

FOMU HII IJAZWE NA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI NA KUREJESHWA SHULENI

TAMKO LA MWANAFUNZI:

1. Mimi NAKUBALI/SIKUBALI kupokea nafasi hii ya kujiunga kidato cha kwanza niliyopewa.
2. Naahidi kufuata na kuyatimiza masharti, kanuni, sheria zote za shule kama inavyoelekezwa na sheria na. 25 ya mwaka 1978 na miongozo inayotolewa na Wizara ya Elimu yenyeh dhamana ya elimu nchini.
3. Niwapo shuleni nitalelewa kwa kufuata misingi ya:
Dini:dhehebu:(kwa ajili ya huduma za kidini)
Jina:..... Sahihi: Tarehe:

TAMKO LA MZAZI:

Mimi: Ambaye ni mzazi/mlezi wa mwanafunzinakili kuwa:

1. Tamko hili limetolewa mbele yangu.
2. Nitashirikiana na shule kulea na kutoa mahitaji yanayotakiwa shuleni kwa wakati muafaka.
3. Nitashirikiana na walimu kufuatilia maendeleo ya mwanagu katika nidhamu na taaluma.

Jina: Sahihi: Tarehe: